

MAANDALIZI YA SIKUKUU YA KUZALIWA MAMA BIKIRA MARIA

NOVENA: 30 August – 7 Septemba, 2019

I SALA KWA ROHO MTAKATIFU

Uje Roho mtakatifu,uzienee nyoyo za waumini wako,peleka roho wako,vitaumbwa vipya na nchi zitageuka.

Tuombe;

Ee Mungu uliyefundisha nyoyo za waumini wako,kwa kuwaletea mwanga wa roho mtakatifu,tunaomba utuongoze na yule roho,tupende yaliyo mea na tupate daima faraja zake,Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo bwana wetu AMINA.

II NIA ZA NOVENA

Kuliombea Kanisa Takatifu la Mungu na Viongozi wa Kanisa

III ROZARI TAKATIFU (Rozari ya siku)

IV LITANIA YA MAMA BIKIRA MARIA

VI SALA YA KUOMBA ULINZI WA MAMA BIKIRA MARIA

Mama wa Mungu, Bikira Maria/ Unikubali ninapokujia
Mimi ni wako, nikiwa mzima/ Mimi ni wako nikizimia
Mimi ni wako, katika mateso/ Mimi ni wako katika misiba
Mimi ni wako, uwapo msalaba/ Mimi ni wako kwa sasa na daima
Mama wa Mungu Bikira Maria/ Unikubali ninapokujia
Mama nakutumainia/ nakutegemea
Mama nakung'ang'ania/ nakulalamikia
Mama mwenye huruma unisimamie / Mama mwenye
uwezo,unihurumie
Uje Mama, unisaidie kusali/ Uje Mama, unisaidie vitani
Uje Mama, unisaidie taabani/ Uje Mama, kaa nami kila mahali
Unaweza kunisadia/ wewe mwezaji
Unapenda kunisaidia/ mwenye upole
Yakupasa kunisaidia/ mwenye huruma
Mama wa neema, msaada wa wakristo/ Makimbilio ya wakosefu

Mlango tunamotafuta wokovu/ Matumaini yetu duniani
Pambo la mbingu la watakatifu/ Wewe ni tuzo la wenye uchungu.
Nani amekuomba, asipate msaada wako?
Lini umedharau, sala za watoto wako,
Nazidi kulia, katika mateso na taabu
Daima Maria, aleta misaada ya ajabu
Katika misiba, nikiwa kufani, nalia
Daima, po pote, ee Mama Maria, saidia .
Ninayo imani na matumaini moyoni,
Maria anipa furaha za mbingu, mwishoni.
Mama wa Mungu, Bikira Maria/ Unikubali ninapokujia
Mimi ni wako, nikiwa mzima/ Mimi ni wako, nikizimia.
Mimi ni wako, katika mateso/ Mimi ni wako, katika misiba.
Mimi ni wako, uwapo msalaba/ Mimi ni wako, kwa sasa na daima.
Mama wa Mungu, Bikira Maria/ Unikubali, ninapokujia.

VII TUNAKIMBILIA ULINZI WAKO

VIII WIMBO: **BIKIRA MARIA MAMA WA MUNGU KWELI**

**/Bikira Maria Mama wa Mungu kweli, ulizaliwa
pasipokuwa na dhambi x2/**

1. Hakuna mwanamke mwingine duniani, aliyebarikiwa kama ulivyo, twakusifu tunakuheshimu.
2. Malaika mbinguni wasifu jina lako, na duniani kote tunalitaja, utamu wa jina hauishi.
3. Sifa zako zavuma popote duniani, jinalo twalitaja tukitetema, njoo kwetu uishi na sisi.
4. Twataka kukuona lakini hatuwezi, kwa kuwa tu wanyonge na wenye dhambi, uzisikilize sala zetu.